


Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 04 Issue: 01 | May-2025

EAJK

# UWINGI-TAALUMA WA BEMBELEZI ZA WASWAHILI

**Authors**
**Lina Akaka** [(1)]; **Jane Maithya** [(2)]
**Main author's email:** akakalina2016@gmail.com

**(1) Daystar University, Kenya; (2) Murang'a University of Technology, Kenya**

**Cite this article in APA as;**
Akaka, L., & Maithya, J. (2025). Uwingi-taaluma wa bembelezi za waswahili. *Eastern Africa journal of kiswahili*, *4*(1), 1-10. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.737

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2025-03-17
Accepted: 2025-04-19
Published: 2025-05-19

**Scan this QR to read the paper online**

**Copyright**: ©2025 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY NC SA) and their terms and conditions.

## IKISIRI

Dhana ya uwingi-taaluma ina maana ya kuunganisha au kuhusisha ujuzi anuwai wa kitaaluma katika mtazamo wa mada au tatizo. Mkabala wa uwingi-taaluma hulenga kueleza tatizo nje ya mipaka ya kawaida kwa kuungwa mkono na mikabala tofauti kutoka taaluma mbalimbali na kufikia suluhu zilizo na misingi yake katika uelewa wa hali changamano (Koski na Savolainen, 2016). Bembelezi za Waswahili zinaakisi uchangamano huo; kwamba zinaonekana kuwa na majukumu anuwai katika jamii. Majukumu kama vile ya utakasaji hisia, mawasiliano, uelimishaji halikadhalika uadilishaji. Majukumu haya ndio yanayoibua hisia kwamba zina uwingi-taaluma na hivyo kuwavutia watafiti kuchunguza taaluma mbalimbali zilizomo. Utafiti uliongozwa na nadharia ya uwingi-taaluma kwa mujibu wa Al-Saleem (2018). Data za bembelezi za Waswahili zilikusanywa katika Kisiwa Faza. Washiriki 11 wa kike wenye umri kati ya miaka 18 na 65 waliteuliwa kwa kuelekezwa na mmoja akateuliwa kimaksudi ili kusailiwa. Vikundi lengwa viwili vya mjadala, kila kimoja kikiwa na wasailiwa sita viliundwa kwa misingi ya umri, na data ya bembelezi 20 ikakusanywa kutokana na vikundi hivyo. Hatimaye bembelezi 10 ziliteuliwa kimaksudi ili kuchunguza uwingi taaluma uliomo. Data zilichanganuliwa kimaelezo. Matokeo ya utafiti yalionyesha dhahiri kwamba bembelezi zina uwingi-taaluma na hutumiwa katika miktadha ya shule, nyumbani, matibabu na mingineyo. Utafiti huu unatoa mchango wa kiusomi kwa watafiti wajao wa fasihi simulizi, wataalamu wa masuala ya elimu, wahudumu wa afya, wanasaikolojia na wanataaluma wengineo hususan wa taaluma zilizoshughulikiwa katika makala haya.

**Maneno Muhimu:** Bembelezi, mlezi, tamaduni, uwingi-taaluma, waswahili.

**UTANGULIZI**

Tangu jadi, bembelezi zimekuwa zikitumiwa na walezi kubembeleza watoto lakini; uchunguzi wa kina wa nyimbo hizi unaonyesha kuwa zina sifa nyinginezo. Sifa hizo zinafichua uwingi-taaluma uliomo ambao utafiti huu unachunguza. Bembelezi huimbwa na wanawake. Akina mama huwaimbia watoto bembelezi ili kuwatuliza wanaposumbua au kuwabembeleza ili walale. Muundo wake ni wa kishairi, zina mishororo na mizani. Sifa zake za kishairi huzifanya ziimbike kwa melodia inayotuliza watoto, (Gunes na Gunes, 2012). Kwa muda mrefu, hususan kabla ya utafiti wa kimaabara, bembelezi zilionekana tu kama nyimbo za kubembeleza watoto haswa katika utamaduni wa Kiafrika. Watafiti wa Kimagharibi walianza kuzichunguza katika maabara na wakagundua kuwa zina sifa zinazoweza kutumiwa katika matibabu. Awali jamii mbalimbali ulimwenguni zilikuwa zikizitumia kuelimisha, kufunza lugha na kupitisha utamaduni wa jamii.

Majaribio mengi ya kimaabara ya bembelezi hususan katika mataifa ya Kimagharibi yamedhihirisha mwingiliano wake na taaluma za matibabu, saikolojia, muziki, elimu na kadhalika. Baadhi ya tafiti hizo ni za Friedman na wenzake (2010), Gunes na Gunes (2012) na Standley (2002). Iwoketok (2009) anasema kuwa bembelezi za Kiafrika zimetafitiwa kwa kiasi kidogo sana. Anahoji kuwa zimepuuzwa kwa sababu ya sifa za ufupi za bembelezi za Kiafrika pamoja na urudiaji wa maneno. Tafiti za bembelezi za Kiafrika zinaonyesha hazijafanyiwa utafiti wa kimaabara, watafiti waliotafiti baadhi ya bembelezi za jamii za Kiafrika walizikusanya nyanjani na kuchanganua yaliyomo**.** Tafiti zao zilichunguza vipengele vya kitamaduni na kielimu vilivyomo mbali na kuchanganua matumizi ya lugha, maudhui na miundo. Bembelezi za Waswahili zina majukumu mbalimbali katika jamii. Hutumiwa kupitisha utamaduni kutoka kizazi hadi kingine, kutakasa hisia hasa za mlezi aliye na msongo wa mawazo, kuadilisha, kushauri, kuelimisha halikadhalika kubembeleza mtoto (Akaka na Wandera, 2022).

Majukumu haya ndio yaliyoleta hisia kuwa huenda mna taaluma nyingine zilizomo mbali na kuwa tu fasihi simulizi. Ilibainika kuwa, mlezi anapomwimbia mtoto bembelezi kwa nia ya kumtuliza, maneno yaliyomo hukusudiwa mtu mwingine. Yaani mlezi huwa anapitisha ujumbe kwa mtu tofauti, anapofanya hivyo, huzifanya bembelezi kuwa jukwaa la mawasiliano. Isitoshe, wakati mwingine mlezi anapomwimbia mtoto, husema yote yanayomkera moyoni na kutakasa hisia zake, hivyo kuibua taaluma ya saikolojia.

Kimsingi kitanzu hiki cha fasihi simulizi hakijatafitiwa sana nchini Kenya kama zilivyotafitiwa nyimbo za michezo ya watoto na ushairi wa watoto. Pengine kilipuuzwa kwa sababu ya urudiaji mwingi wa maneno mishororo na vifungu vya maneno. Hata hivyo, bembelezi za Waswahili zina mengi yaliyomo ambayo yanafunza, kutakasa, kutuliza, kuelimisha na kadhalika. Jambo hili linazifanya ziwe na uwingi-taaluma ambao utafiti huu ulichunguza.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Nettl (2005) anaonyesha kuwa bembelezi ni aina ya muziki bia ambamo mna taaluma nyinginezo. Kulingana naye, majukumu yake ya kiutamaduni, kiutendakazi na kihisia huzipa sura ya uwingi-taaluma. Kwa mtazamo wa kiethinomuziki, anasisitiza kuwa bembelezi sio tu tungo za kisanaa ila hutumika katika majukumu ya kiutendaji kama vile kubembeleza watoto na kujenga ukaribu nao mapema. Nettl anaongeza kuwa miundo sahili ya bembelezi huibua suala la utambuzi wa muziki na saikolojia ya ukuaji wa mtoto. Masuala hayo yakiwemo takriri, melodia nyororo na mahadhi ya chini hutuliza ubongo wa mtoto. Sauti taratibu na nyororo ya kurudiwarudiwa hutuliza mtoto.

Nettl (2005) anahoji kuwa, utambuzi wa muziki hueleza ni kwa nini sauti hizo hutuliza. Nettl alichunguza pia vile bembelezi zinavyoakisi kaida za kitamaduni hivyo akazihusisha na taaluma ya anthropolojia. Isitoshe alisema maneno yaliyomo yalifichua jumbe za kijamii au wasiwasi wa mama dhidi ya mtoto hivyo akazihusisha na taaluma za jinsia, fasihi andishi na simulizi. Hivyo, Nettl anaonyesha uwingi-taaluma uliomo katika bembelezi.

Golinkoff na Hirsh-Pasek (2000) walichunguza mchango wa bembelezi kwa ukuaji wa mtoto hususan katika upataji wa lugha. Golinkoff na Hirsh-Pasek wanasema kuwa bembelezi ni muhimu sana kwa mtoto katika ujifunzaji wa mapema wa lugha. Wanaeleza kuwa walezi wanapoimba, wanajipata wakitumia maneno sahili ambayo mtoto anaweza kuelewa haraka na huimba kwa njia inayovutia mtoto.

Melodia rahisi wanayotumia, mahadhi ya chini na urudiaji wa maneno husaidia mtoto kutambua ruwaza katika sauti ambayo ni hatua muhimu katika kujifunza kuzungumza. Waandishi hawa wanasisitiza kuwa uimbaji wa bembelezi huimarisha ukaribu wa kihisia kati ya mtoto na mlezi. Huunda mazingira salama ya kuanzisha mawasiliano mapema kati yao. Mtazamo wa uchunguzi wa bembelezi uliofanywa na Golinkoff na Hirsh-Pasek (2000) ni wa saikolojia ya ukuaji wa mtoto.

Katika utafiti wa Standley (2002), alichunguza athari ya therapia ya muziki, bembelezi zikiwemo kwa watoto waliozaliwa kabla ya mama kufikisha siku ya kujifungua. Watoto hao waliwekwa kwenye vitengo vya malezi ya watoto wachanga na kuimbiwa bembelezi zilizorekodiwa. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa bembelezi na muziki mwingineo uliokuwa na melodia na mahadhi ya chini kama ya bembelezi uliboresha utendakazi wa viungo muhimu mwilini kama vile kiwango cha mpigo wa moyo, viwango vya oksijeni, kuboresha jinsi walivyokula na kuzidisha uzani wa mwili. Standley aligundua pia kuwa bembelezi zilisaidia kupunguza mfadhaiko katika watoto wachanga. Matokeo ya utafiti wake yalisisitiza nguvu za kitherapia zilizomo katika muziki wenye melodia na mahadhi taratibu yanayotuliza hususan katika tiba ya watoto wachanga. Utafiti huu ulionyesha kipengele cha taaluma ya tiba kilichomo kwenye bembelezi.

Friedman na wenzake (2010) walichunguza matumizi ya therapia ya bembelezi zilizorekodiwa kwa ugonjwa wa kiakili unaowakumba akina mama baada ya kujifungua na akina mama wajawazito. Sampuli yao ya utafiti ilikuwa akina mama wajawazito 48 waliokuwa na mfadhaiko wa akili, *bipola* au saikosisi na waliokuwa wamemaliza siku chache baada ya kujifungua. Wasailiwa hawa walisikiliza bembelezi kwa muda wa wiki mbili huku viwango vya utulivu vikirekodiwa kwa mashine. Waliweza kuona tofauti siku ya tatu baada ya kuanza therapia hiyo na baada ya muda wa wiki mbili, utulivu ulikuwa umerudi kikamilifu. Ishara na dalili za ugonjwa wa kiakili zilipungua baada ya akina mama hao kusikiliza bembelezi zilizorekodiwa. Utafiti huo ulibaini uwingi-taaluma uliomo katika bembelezi.

Utafiti wa Akaka na Wandera-Simwa (2022) unaonyesha kuwa bembelezi zilitumiwa na wanawake Watikuu nchini Kenya kama jukwaa la mawasiliano. Akaka na Wandera-Simwa walichunguza walengwa wa ujumbe uliomo katika bembelezi za wanawake Watikuu nchini Kenya na kubaini kuwa walezi huzitumia kupitisha ujumbe kwa wanajamii mbalimbali huku mtoto akifaidi tu kutokana na melodia ya bembelezi hizo. Iwapo pangekuwa na mwanajamii aliyemkosea mlezi, mlezi huyo aliyatoa yaliyokuwa moyoni mwake kupitia kwa bembelezi na mlengwa wa ujumbe katika bembelezi alijibu pia kwa bembelezi nyingine. Baadhi ya wanajamii waliolengwa na ujumbe uliomo ni mume wa mlezi, wifi zake, mama mkwe, ndugu za mtoto, jirani halikadhalika mtoto mwenyewe. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa mbali na nyimbo hizi kutumiwa kubembeleza watoto, zilitumiwa na wanawake pia kama jukwaa la mawasiliano. Utafiti huo ulibaini kuwa taaluma ya mawasiliano imo katika bembelezi hivyo kuonyesha uwingi-taaluma wake.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulifanywa katika Kisiwa cha Faza. Vikundi lengwa vya utafiti vilikuwa wanawake Waswahili na bembelezi za Waswahili. Msailiwa mmoja wa kike aliteuliwa kimaksudi na wasailiwa 11 wakateuliwa kwa mbinu ya uteuzi wa sampuli ya kuelekezwa ili kushirikishwa katika utafiti. Wasailiwa waligawanywa katika vikundi lengwa viwili vya mjadala kwa misingi ya umri. Kikundi cha kwanza kikiwa na wasailiwa wenye umri kati ya miaka 25-40 na kikundi cha pili kikiwa na wasailiwa wenye umri kati ya 41-68.

Data za bembelezi 20 zilikusanywa kutoka vikundi hivi, kila kimoja kikitoa bembelezi 5 10 na bembelezi 10 zikateuliwa kimaksudi ili kutafitiwa. Vifaa vilivyotumiwa kukusanya data ni kalamu, daftari na kifaa cha kunasa sauti. Watafiti walisikiliza data zilizokuwa zimenaswa katika kifaa cha kunasa sauti na kuzinakili kisha wakazichunguza na kubaini taaluma mbalimbali zilizomo katika bembelezi za Waswahili.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Ilibainika wazi kuwa bembelezi za Waswahili zimesheheni taaluma mbalimbali. Baadhi ya taaluma hizo ni fasihi, elimu, isimu, saikolojia, historia au utamaduni na mawasiliano. Iligunduliwa kuwa majukumu tofauti yaliyo nazo nyimbo hizi yameibua taaluma mbalimbali zilizomo kama ilivyotajwa awali. Hivyo matokeo ya utafiti yalidhihirisha wazi kuwa

bembelezi za Waswahili zina uwingi-taaluma kama ilivyojadiliwa katika sehemu zifuatazo.

**Taaluma ya Elimu**

Kabla ya majilio ya Wazungu barani Afrika, Waafrika walikuwa wakielimisha na kuadilisha watoto kupitia kwa simulizi zao. Vipera mbalimbali vya fasihi simulizi kama vile ngano, ushairi simulizi ambao bembelezi ni miongoni mwa vijipera vyake, semi halikadhalika mawaidha vilitumiwa kuelimisha watoto kando na kuburudisha jamii kwa jumla. Mosweunyane (2013) anahoji bara la Afrika lilikuwa na mfumo wake wa mafunzo na ujifunzaji kabla ya kipindi cha ukoloni pia kabla ya majilio ya wamishenari.

Mosweunyane anaendelea kufafanua mifumo ya mafunzo ya Waafrika. Anasema shule za kitamaduni zilikuwepo na kitengo cha familia na jamii kilitumika kama mfumo muhimu wa kutoa na kupata maarifa, uadilishaji na kupitisha amali na utamaduni wa jamii. Watoto walimilikiwa na jamii, na masuala ya mafunzo na nidhamu yalishughulikiwa na watu wazima, hata kama hawakuwa jamaa za mtoto (Kipkorir, 1987). Kipkorir anaendelea kuhoji kuwa, jamii nzima ilishiriki katika mchakato wa elimu ili kuandaa watoto kwa maisha ya utu uzima. Kupitia kwa mchakato huu wa elimu ambao haukuwa na utaratibu wowote, watoto wa kiume walifunzwa masuala ya kiume na wasichana wakafunzwa masuala ya uke na ulezi. Katika ubeti ufuatao wa bembelezi ya Waswahili, mama akimwimbia binti yake anamhimiza kukua ili akishakua afundishwe unyumba na kumtunza mumewe:

*Howa nchoncho, howa x2*
*Kuwa mkubwa mwanangu*
*Rukiya nikuelimishe*
*Nikufundishe unyumba, umtunze mume*

Aina ya elimu inayopatikana katika bembelezi ni elimu ya kimaadili na kitamaduni na hili linajitokeza sio tu katika bembelezi za Waswahili bali za jamii nyingine za Kiafrika kama inavyodhihirika katika utafiti wa bembelezi za Nigeria uliofanywa na Iwoketok (2009) na Ebeogu (1991). Waswahili waliwaelimisha na kuwaadilisha watoto wao kupitia kwa bembelezi. Kando na elimu ya Kimagharibi, Waswahili wangali wanawafunza watoto kupitia kwa simulizi zao tangu utotoni hata kabla kufikia miaka ya kuanza shule. Mojawapo ya simulizi hizo ni bembelezi; nyimbo ambazo watoto huimbiwa na walezi wanapokosa utulivu kwa sababu ya kuhisi njaa, usingizi au mfadhaiko wa aina yoyote.

Waswahili kupitia kwa bembelezi waliwaeleza watoto majukumu yao katika jamii. Mama au mlezi alimweleza mtoto matarajio ya jamii kumhusu; mama alimweleza kuhusu kilimo, uchungaji mifugo na kazi nyinginezo kupitia kwa bembelezi, kwa mfano:

*Howa nchoncho, howa x2*
*Ukenda hondeni tukuwa bori na daba*
*Na vunga vako taani japokuwa ni kibaba*
*Usiatie ruhuni yatakuvua mahaba*

Haya yanadhihirika katika utafiti wa bembelezi za Watikuu uliofanywa na Akaka na wenzake (2021). Hali hii inajitokeza pia katika bembelezi za Nigeria, Iwoketok (2009) anaposema, bembelezi za Kiafrika zilitumiwa kuelimisha watoto kuhusu utamaduni wa jamii zao.

**Taaluma ya Isimu**

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha na matendo kuwasilisha ujumbe juu ya maisha ya binadamu (Simiyu, 2011). Matumizi ya lugha katika matini yoyote yanaweza kuchanganuliwa kwa kiwango cha kiisimu ama kifasihi. Lugha inayotumiwa katika bembelezi inaweza kuchanganuliwa kwa kiwango cha kiisimu kwa kuchunguza miundo ya kisintaksia ya sentensi zilizomo, sauti na msamiati uliomo. Nakin (2021) anaeleza fasihi ya watoto ni muhimu kwa kuwa ndio chanzo cha ulimwengu wa kiasili na lugha elezi kwa watoto, inaboresha msamiati, kupanua maarifa na uelewa wao.

Nakin akiwanukuu Martini na Granqvist (1997), anasema wanaunga mkono wazo lake wanaposema ruwaza za sauti zilizomo katika bembelezi hunasa mawazo ya mtoto. Baadhi ya ruwaza hizo ni miundo ya kisarufi, ambayo mara nyingi hujumuisha uwiano wa vokali, urudiaji, takriri, tanakali za sauti halikadhalika vitanza ndimi. Bembelezi za Waswahili zimesheheni sifa za kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia. Urudiaji ambao Hala na Bezo (2022) wanahoji ndio kipengee muhimu cha simulizi za watoto, umo katika bembelezi za Waswahili kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao:

*Hongera mwanangu, we hongera nami nihongere*
*Hongera mama uchungu, mama uchungu we*
*Hongera mwanangu tumbo la uvyere linauma*
*Nyamaza zii mwanangu we hoyee*

Ubeti huo una urudiaji wa neno *hongera* mwanzoni mwa mishororo mitatu ya kwanza. Urudiaji ni kipengele muhimu sana cha uratibu katika bembelezi. Njia hii ya kujenga beti kwa kutumia kipengele cha urudiaji huipa neno umuhimu wa kisemantiki na kuimarisha jinsi bembelezi zinavyowasilisha mawazo (Hala na Bezo, 2022). Ubeti ulionukuliwa una urudiaji wa sauti za konsonanti mwanzoni mwa maneno. Melodia inayozalishwa na urudiaji huo humtuliza mtoto, (Ulutus, 2022). Kipengele cha sauti ni kimojawapo cha mambo ya kimsingi katika ukuzaji wa ujuzi wa lugha tamkwa. Watoto huanza kusikia sauti katika mazingira yao wakiwa vijusi katika tumbo za mama zao (Moon na Fifer, 2000).

Vipengele vya kimofolojia vinadhihirika katika maumbo ya maneno kwa mfano matumizi ya kiambishi "*–ngu*" *kilichoongezwa* mwishoni mwa neno *mwana* kinaashiria hisia za upendo wa mama kwa mtoto. Urudiaji wa maneno *mama uchungu* unakusudiwa kuvutia hisia za huruma kwa mama. Urudiaji unaobainika katika miundo ya kifonolojia na kimofolojia katika bembelezi za Waswahili huchochea upataji wa lugha ya kwanza (Miyashita, 2011). Kama asemavyo Miyashita (2011), akili ya mtoto mchanga ni yenye uwezo mkubwa wa kufyonza maarifa haraka. Licha ya hilo, hung'amua vipengele vya lugha kwa kasi vinaposisitizwa kwa kurudiwa mara kwa mara.

Kisintaksia, bembelezi za Waswahili kama nyinginezo ulimwenguni hutungwa kwa sentensi fupifupi sahili ambazo hurahisisha uimbaji wake. Mama huzungumza na mtoto kwa kutumia usemi halisi hivyo kumhusisha mtoto moja kwa moja katika mazungumzo yaliyo kwenye bembelezi. Mazungumzo hayo kwa mujibu wa Ulutas (2022) yana nafasi muhimu kwa mtoto katika upataji wa lugha ya kwanza. Kupitia kwa mazungumzo hayo, mama kama mtu anayekimu mahitaji ya kimsingi ya mtoto, huwa na jukumu kubwa la kumfanya mtoto kuutambua na kuuelewa ulimwengu wake.

Kisemantiki, kifungu *mama uchungu* kinaashiria uchungu wa uzazi na kifungu *tumbo la uvyere linauma* kuashiria tumbo la uchungu wa uzazi hivyo kusisitiza ujitoleaji wa mama katika shughuli za malezi. Toni ambayo mama anatumia anapoimba huashiria hisia zinazokinzana; za furaha, aidha uchungu. Sifa za kiisimu hudhihirika katika bembelezi sio tu za Waswahili bali pia za tamaduni nyingine kama inavyobainika katika bembelezi za Wapoli zilizotafitiwa na Sikora na Żebrowska (2013). Iwoketok (2009) anasema simulizi chache za watoto za Kiafrika zilizotambuliwa hususan bembelezi zilifanyiwa uchunguzi unaoonyesha kuwa kando na majukumu ya kubembeleza, huendeleza utamaduni na kukuza lugha ya mtoto. Iwoketok anahoji pia kuwa bembelezi za Kiafrika zimetoa mfano mzuri wa uchunguzi wa kiwingi taaluma.

Isimu ina matawi mengi likiwemo la isimu tambuzi. Tawi hili liliasisiwa na Lakoff na Johnson (1980) na huchunguza uhusiano uliopo kati ya lugha na utambuzi. Michakato ya kiulinganifu baina ya dhana za kidhahania na dhana halisi katika mazingira huundwa katika utambuzi kutokana na tajriba za kimwili na utamaduni, (Lakoff na Johnson, 1980). Wanaendelea kufafanua kuwa, dhana ya kidhahania huelezwa kistiari kwa kuihusisha na dhana katika mawanda halisi. Baadhi ya bembelezi za Waswahili zimesheheni sitiari kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao:

*Howa nchoncho howa x2*
*Bamba ni kitu muhimu kwa kusi na kaskazi*
*Na nyumba pia hudumu hupungua nyingi kazi*
*Waume hujifahamu mambo yote ni wazazi*

*Howa nchocho howa x2*
*Bamba ndilo la kufaa kwa mvua na hata jua*
*Nyumba ni yako haswa kwa mtu atakutowa*

Sitiari *bamba* katika ubeti huo ina maana ya mume, sitiari *kusi* na *kaskazi* zina maana ya hali nzuri na mbaya, sitiari *mvua* na *jua* zina maana ya hali ngumu na nzuri. Sitiari hizo zimelinganishwa na dhana pamoja na misimu katika mazingira ya Waswahili, mazingira ya pepo za bahari na misimu wanayoshuhudia katika mazingira yao.

**Taaluma ya Fasihi**

Bembelezi ni kitanzu cha fasihi simulizi ambacho kina sifa za kifasihi. Baadhi ya vijenzi vya fasihi vinavyodhihirika katika bembelezi za Waswahili ni maudhui yaliyomo, muundo wa kishairi, mandhari

tofautitofauti yanayorejelewa katika bembelezi, matumizi ya lugha ya kifasihi na wahusika. Bembelezi zina vipengele sawia vya kimuundo na kimtindo na simulizi nyinginezo za kifasihi kama vile mashairi simulizi. Lugha inayotumiwa katika bembelezi ni ya kifasihi, lugha iliyosheheni tamathali zinazozitofautisha na kazi nyingine zisizo za kifasihi. Waswahili wana sifa ya kutumia mafumbo katika nyimbo, mashairi na simulizi nyinginezo wanazotumia. Sifa hii inajitokeza katika bembelezi zao pia. Walezi hutumia bembelezi hizo kueleza hisia zao kuhusu suala wanalozungumzia (Akaka na Wandera-Simwa, 2022). Suala hilo huwasilishwa kwa sitiari na ishara mbalimbali kama ilivyo katika ubeti ufuatao:

*Howa nchoncho howa x2*
*Mwanahalima ni bahari amekosa kueleweka*
*Nyumba ujenge jela na milango yake sita*
*Simai huwa umelala na atakaye hupita*

Katika ubeti huo, mshororo wa pili una sitiari inayomlinganisha Mwanahalima na bahari. Mwimbaji anamsuta kwa tabia yake ya kukaribisha kila mwanamume nyumbani mwake. Hivyo anamlinganisha na bahari ambamo kila chombo hupita. Mlezi anaendelea kumsuta Mwanahalima akisema kuwa kila atakaye hupitia hapo. Hivyo kwa kejeli anamhimiza kujenga nyumba iliyo na milango sita ambapo mwanamume anapotumia mmoja kuingia aliye ndani anatumia mwingine kuondoka. Ingawa lugha kama hii inatumiwa katika bembelezi za Waswahili, haikusudiwi mtoto, mtoto hufaidi tu kwa melodia ya bembelezi yenyewe. Ujumbe hukusudiwa mwanajamii anayelengwa. Bembelezi za Waswahili hubeba maudhui changamano ambayo hulenga wanajamii (Akaka na Wandera-Simwa, 2021).

Mandhari tofautitofauti ya pwani yanaakisiwa katika bembelezi hizi, sio ya uvuvi, uwindaji, ukulima na mengineyo. Kwa mfano ubeti ufuatao unaakisi mandhari ya kilimo:

*Nami nilikuwa na matango yangu eeh x2*
*Alitokea hasidi akaukanyaga*
*Naliliya kupata bahati yangu*
*Si bure mambo, nilikuwa na mkorosho wangu*
*Katokea hasidi akauwasha moto, naulilia*

Ubeti huo unaakisi mimea inayopandwa katika mazingira ya pwani. Mlezi anaeleza vile mimea yake ilivyoharibiwa na hasidi, kwanza matango, baadaye mkorosho. Hii ni taswira ya shughuli za kilimo wanazofanya Waswahili. Kwa hivyo, hawana budi kuakisi shughuli hizi katika bembelezi zao. Wakati mwingine walezi hulinganisha vitu katika mazingira yao na tajriba zao za maisha kwa juhudi za kuwafahamisha wanajamii mambo wanayoyapitia maishani.

**Taaluma ya Historia/ Utamaduni**

Historia ni kisa cha mambo yaliyopita na ni kisa kuhusu jamii ya wanadamu, (Ghosh, 2019). Mwandishi huyu anaendelea kufafanua kuwa ni taaluma inayochunguza binadamu sasa na katika nyakati zilizopita kwa misingi ya ithibati. Historia ni aina ya maarifa ya kina yanayosaidia kuelewa jamii ya binadamu na mabadiliko yake. Hurekodi mawazo na shughuli za kijamii za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kidini; kwa maneno mengine, ni daftari kuhusu binadamu na shughuli zake.

Kuna mpaka mwembamba kati ya fasihi na historia. Fasihi hususan simulizi ni chombo kilichobeba historia ya jamii. Wanahistoria, katika harakati za kukusanya na kurekodi historia za jamii mbalimbali, hutumia fasihi simulizi za jamii husika kama vyanzo vya kubaini shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii zilizoendelezwa katika jamii hizo zamani. Gilbert (2005) anasema wanahistoria huchunguza nyimbo ili kutambua maisha ya jamii kiuchumi na kijamii kupitia mpito wa wakati. Bembelezi za Waswahili zinaakisi shughuli hizi mbalimbali na imani yao kuhusu mambo mbalimbali kwa mfano katika ubeti ufuatao:

*Howa nchocho howa x2*
*Silie usiku ndia zina vachu*
*Zina vaswalina na vachavo Mungu*
*Mame mwanangu niombea*
*Mungu siku ya utungu*

Mlezi anamsihi mtoto kunyamaza katika ubeti huo. Anamwambia asilie kwa kuwa usiku njia zina watu, wanaomcha Mungu na wasiomcha. Waswahili hulinda sauti ya mtoto haswa usiku, huizuia isisikike nje kwa sababu wana imani kuwa ndege mbaya au hata watu wabaya wasiomcha Mungu wanaweza kuichukua sauti ile na kumdhuru mtoto. Imani hii inayowalinda watoto kutokana na mahasidi inazingatiwa pia katika jamii ya

Waswahili wa Unguja. Kwa mujibu wa Mbayi (2009), katika uchanganuzi wa *Utenzi wa Howani Mwana Howani* alibaini kwamba mama mjamzito anapokaribia kujifungua, akina mama walijaa ukumbini ili mtoto anapotoka tumboni na kulia, akina mama hao wanapiga vigelegele na kuzamisha ile sauti ili isije ikapenya na kuenea mitaani.

Kimsingi, mwono-ulimwengu wa Waswahili hudhihirika katika bembelezi zao. Mwono-ulimwengu huo ndio huumba imani, tamaduni, amali na historia yao. Mwono-ulimwengu wa jamii yoyote ile hutokana na mazingira na hili hudhihirika katika msamiati wanaotumia katika simulizi zao. Msamiati huo huakisi mazingira yao kama inavyobainika katika bembelezi za jamii nyinginezo ulimwenguni. Kwa mfano bembelezi zinazoimbwa katika mataifa ya Kimagharibi zimesheheni misamiati inayoakisi mazingira yao; misamiati kama vile dubu na theluji; dhana zisizopatikana katika mazingira ya Kiafrika. Mwingiliano kati ya kitanzu cha fasihi simulizi cha bembelezi na utamaduni pamoja na mazingira hukipa mkabala wa uwingi-taaluma.

Utamaduni wa ndoa za Waswahili unajitokeza katika bembelezi hizi. Kwa mfano inabainika kuwa mwanamume anaweza kuoa zaidi ya mke mmoja kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao:

*Si bure mambo, usiku wa jana*
*Nilihangaika kuandaa chai ndani ya*
*Birika eeh, nilidhani ni wangu kumbe*
*Ni wa shirika*

Aluede na Abu (2005) wanahoji nyimbo za kitamaduni zimefungwa kwenye utamaduni ambamo zimetungwa na watu wasiojulikana na kupitishwa kutoka kizazi hadi kingine na waimbaji. Bembelezi za Waswahili zinaakisi utamaduni ambamo mabinti katika jamii hii huozwa kwa wanaume ambao wazazi wao wamewachagulia. Isitoshe wasichana wanapokaribia kubaleghe huanza kufundishwa unyumba ili waandaliwe kwa maisha ya ndoa. Wasichana hawakuruhusiwa kushiriki tendo la ndoa kabla ya kuolewa na yeyote aliyefanya hivyo alikuwa na hatari ya kukosa mume.

**Taaluma ya Mawasiliano**

Uhusiano baina ya mawasiliano na bembelezi huwa kwenye majukumu yake kama wenzo wa kupitisha ujumbe, hisia na maadili ya kiutamaduni. Kimsingi, katika utamaduni wa Waafrika, Waswahili wakiwemo, nyimbo zilitumiwa kama jukwaa la mawasiliano. Katika bembelezi ifuatayo, mlezi anamkashifu rafiki yake kwa kosa alilomfanyia. Mlezi anasema alimfanya rafiki, akampa siri za ndani kumbe huku rafiki yake alikuwa akimla ndani kwa ndani.

*Howa Nchocho Howa x2*
*Nilikufanya rafiki kakupa siri za ndani*
*Kisha kakufanya wanda kakutia matoni*
*Karama uwe ni simba hunila ndani kwa ndani*

Katika tamaduni nyingi ulimwenguni, bembelezi huwa jukwaa la mawasiliano baina ya mlezi na mtoto anayebembelezwa. Kwa mujibu wa Hala na Bezo (2022), bembelezi hupitisha hisia kama vile upendo, malezi na faraja kutoka kwa mlezi hadi kwa mtoto. Toni, melodia na rithimu husaidia kudhibiti hisia za mtoto na kuunda uhusiano wa dhati baina ya mlezi na mtoto. Licha ya hayo, Waswahili pia hutumia bembelezi kuwasilisha hoja sio tu kwa mtoto bali kwa wanajamii mbalimbali. Walezi huwalenga wanajamii mbalimbali wanapoziimba, (Akaka na Wandera-Simwa, 2022).

Walengwa wa ujumbe uliomo katika bembelezi za Waswahili huwa waume, mama wakwe, akina wifi, majirani na wanajamii wengineo. Diskosi hizo hufumbwa kwenye mafumbo kama ilivyo desturi ya Mswahili kutumia nyimbo kutoa dhiki alizo nazo moyoni. Chiraghdin (1973) katika Abdalla (2012), anashadidia kauli hiyo anaposema kuwa, "Na kwa Mswahili, njia nzuri zaidi ni ya kutongoa kwa mashairi na nyimbo, akiwa ajua," (Abdalla, 2012:vi). Si ajabu bembelezi za Waswahili ni jukwaa la mawasiliano ambalo hutumiwa na walezi kubeza, kukanya, kuonya na kukemea wanajamii mbalimbali waliotofautiana nao. Sifa hii, haidhihiriki tu katika bembelezi za Waswahili. Nakin (2021) anaeleza kuwa, katika baadhi ya tamaduni, bembelezi hutumiwa na wanawake kueleza kutoridhika kwao katika ndoa.

**Taaluma ya Saikolojia**

Bembelezi zinaweza kuakisi hali ya kisaikolojia ya mlezi. Majd na Bakhashaliyev (2016) wanahoji bembelezi zinazoimbwa na akina mama huhusishwa na hisia za malalamiko, upweke, wasiwasi na kutoridhika kutokana na matatizo ya kijamii na

kiuchumi. Hali hii inabainika katika bembelezi za Waswahili ambapo walezi huzitumia kutakasa hisia zao. Aghalabu mume anapomkosea mke wake, mke hutumia fursa ya kubembeleza mtoto kuimba bembelezi ambayo ujumbe uliomo humlenga mume wake. Kwa mfano, ujumbe katika bembelezi ifuatayo unamlenga babake mtoto:

*Howa mtoto howa x2 Silie mwana, silie eeh*
*Ukilia waniliza, wanikumbusha ukiwa wa baba na mama. Baba na mama katenda, kanioza dume kongwe. Halisafiri halendi kazi, kazi kumeza matonge*

Ujumbe katika bembelezi hiyo unaonyesha msongo wa mawazo alio nao mama huyu. Anaeleza kuwa aliozwa huyu mume na wazazi wake na mume mwenyewe ni mvivu, kazi yake ni kula tu. Hivyo amemwachia mke wake majukumu ya nyumbani. Jambo hili linaonekana kumtatiza kisaikolojia, hivyo anatumia bembelezi kueleza hisia alizo nazo dhidi ya mume wake na kutakasa hisia zake. Tafiti za bembelezi za tamaduni nyingine zimebaini umuhimu wa bembelezi katika masuala ya kisaikolojia. Majd na Bakhshaliyev (2016) wanasema bembelezi za akina mama wa Iran aghalabu huwa bubujiko lililofichika katika sehemu ya ndani ya wanawake kwenye jamii ya Wairan.

Msongo wa mawazo, wasiwasi na matatizo mengine ya kisosholojia na kisaikolojia yanayotokana na hali ya wanawake nchini hum.o Matatizo yanayohusiana na kutokuwepo kwa baba nyumbani, ndoa yake ya pili na upweke umesababisha akina mama kukosa mwandani isipokuwa watoto wao hivyo kutumia bembelezi kujituliza kwa kueleza hisia zao. Si ajabu Akaka na Wandera-Simwa (2022) wanahoji kuwa katika baadhi ya bembelezi za Waswahili, maneno yaliyomo hulenga wanajamii wengine huku mtoto akifaidi tu kwa melodia ambayo humbembeleza akatulia.

Katika mataifa ya Kimagharibi, bembelezi hutumiwa kitherapia katika matibabu ya magonjwa wa kiakili. Katika tafiti zilizofanywa kuhusiana na masuala ya kiakili iligunduliwa kuwa therapia ya bembelezi kwa akina mama iliwapunguzia dalili za magonjwa ya kiakili kama wanavyosema Friedman na wenzake (2010). Baadhi ya akina mama hukumbwa na ugonjwa wa kiakili baada ya kujifungua na hupata nafuu na utulivu baada ya kusikiliza bembelezi. Hivyo bembelezi huingiliana na saikolojia na kuzifanya ziwe na uwingi taaluma zinapotumiwa kama therapia ya magonjwa ya kiakili.

**Taaluma ya Muziki**

Umuziki wa bembelezi hutokana na mchanganyiko wa melodia, rithimu, takriri na vipengele vinginevyo vya kishairi. Bembelezi zina vipengele vingi vya kimuziki vinavyojumuisha melodia sahili, miundo ya kiuradidi na rithimu nyororo ambazo huunda athari za kutuliza (Malloch na Trevarthen, 2009). Sifa zake za kimuziki huzifanya ziwe rahisi kukumbukwa na kuimbika. Mojawapo ya kipengele cha umuziki wa bembelezi ni maneno yaliyomo ambayo hujengeka kwa vipengele vya kishairi kama vile takriri ya sauti za vokali na konsonanti pamoja na vina. Vipengele hivi huzalisha kiwango cha ubora wa melodia ya bembelezi na kuzifanya kukumbukwa kwa wepesi na hivyo kupitishwa kutoka kizazi hadi kingine. Toni nyororo na utamkaji wa maneno kwa ulaini pia huongeza athari ya utulivu kwa mtoto.

Sifa hizo ni zenye ruwaza za kiuradidi katika sauti, maneno na vifungu vya maneno yaliyomo. Sifa hizi huibua hisia vile tu unavyoibua muziki. Bembelezi hujenga uhusiano wa karibu baina ya mlezi na mtoto, Isitoshe huleta utulivu, usalama na udhibiti wa kihisia. Kimsingi muziki wowote ule huleta athari hizo, Na kuakisi kaida za kitamaduni, maadili na historia ya jamii husika. Bembelezi zina sifa hizo; hubeba ujumbe, imani na kaida za kipekee za jamii husika kama ulivyo muziki mwingine wowote ule.

Kama muziki, bembelezi husaidia katika upataji wa lugha na kujenga utambuzi. Ruwaza za kimelodia na kirithimu katika bembelezi humsaidia mtoto kutambua sauti, kujenga uwezo wa kuzungumza na kuboresha kumbukumbu. Muziki, zikiwemo bembelezi, hutumiwa katika therapia ili kupunguza msongo wa mawazo na kusaidia kuleta usingizi (Ibekwe na Umezinwa, 2017). Sifa za kutuliza za bembelezi zinalingana na matumizi pana ya muziki kitherapia katika kutuliza na kuponya (Sugiyama, 2001).

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Makala hii imeonyesha taaluma mbalimbali zilizomo katika bembelezi za Waswahili. Uwingi taaluma wake hutokana na mikabala anuwai iliyomo ya kiisimu, kifasihi, kisaikolojia, kielimu, kiutamaduni na

kijamii. Isitoshe, kuwepo kwa uwingi-taaluma huo kunaangazia pia sura mbalimbali za majukumu ya bembelezi katika jamii. Mikabala ya kifasihi, kiisimu, kisaikolojia, kielimu, kitamaduni na kihistoria katika bembelezi za Waswahili huonyesha umuhimu wake ambao ni zaidi ya nyimbo za kutuliza watoto tu.

Mikabala tofauti ya bembelezi inapanua matumizi yake katika miktadha ya nyumbani. Hivyo licha ya kubembeleza watoto, maudhui yaliyomo hutumiwa kuadilisha, kushauri na kuelimisha. Utafiti umeonyesha kuwa bembelezi zinaweza kutumika katika ufundishaji wa wanafunzi wa chekechea, shughuli za utafiti, kutuliza akili zilizosongwa na mawazo halikadhalika kama jukwaa la mawasiliano. Bembelezi kama hazina ya utamaduni wa jamii huhifadhi lugha na kuendeleza mitagusano ya wanajamii wanapozitumia kama jukwaa la mawasiliano. Uwingi-taaluma uliomo unasisitiza umuhimu wa kutambua bembelezi kama chombo muhimu cha utamaduni ambacho huakisi na kuumba utambulisho na amali za jamii ya Waswahili. Itakuwa bora zaidi iwapo zingetafitiwa katika maabara ili kutambua thamani yake katika matibabu ya aina tofauti za magonjwa hususan wa kiakili.

**Mapendekezo:** Bembelezi za Waswahili zina hazina kuu ya uwingi-taaluma kama matokeo ya utafiti yalivyoonyesha. Kila taaluma ichunguzwe kwa kina katika bembelezi za Waswahili na bembelezi za jamii nyinginezo nchini ili zitumike kwa shughuli za tiba mahospitalini, katika taaluma ya saikolojia ya ukuaji wa watoto, sekta ya elimu na nyinginezo. Bembelezi za jamii mbalimbali zikusanywe na kurekodiwa kwa ajili ya tafiti zijazo za bembelezi kwa kuwa zinaendelea kupotea kutokana na teknolojia.

**MAREJELEO**


Abdalla, A. (2012). *Sauti ya dhiki*. Oxford University Press.

Akaka, L., & Wandera, S. (2022). Walengwa wa ujumbe katika bembelezi za Watikuu. *East African Journal of Swahili Studies, 5*(1), 288–296.

Akaka, L., Wandera-Simwa, S., & Onyango, J. O. (2021). Maudhui katika bembelezi za wanawake Watikuu nchini Kenya. *Editon Consortium Journal of Kiswahili, 3*(1), 211–222.

Al-Saleem, N. E. (2018). Historical development of the interdisciplinary studies. In *Promoting interdisciplinarity in knowledge generation and problem solving* (pp. 222–233). IGI Global.

Aluede, C. O., & Braimah, A. A. (2005). Edo folksongs as sources of historical reconstruction. *Studies of Tribes and Tribals, 3*(2), 123–128.

Banerjee, S. (2021). Embracing multi-disciplinarity and innovation: Emerging trends in English literature research. *IOER International Multidisciplinary Research Journal, 3*(2), 25–33.

Ebeogu, A. (1991). The world of lullaby: The Igbo example. *Research in African Literatures, 22*(2), 99–117.

Friedman, S. H., Kaplan, R. S., Rosenthal, M. B., & Console, P. (2010). Music therapy in perinatal psychiatry: Postpartum women with mental illness. *Music and Medicine, 2*(4), 219–225.

Ghosh, S. (2019). An introduction of history. *IJARIIE, 5*(4), 713–716.

Golinkoff, R. M., & Hirsh-Pasek, K. (2000). *How babies talk: The magic and mystery of language in the first three years of life*. Penguin.

Hala, M., & Bezo, B. H. (2022). Lullabies, language analysis and features. *Polis, 21*(1), 150–168.

Ibekwe, E. U., & Umezinwa, E. C. (2017). The rhythmic sensibility of African folksongs: The case of lullabies in Igbo culture. *African Journal of Arts and Humanities, 3*(5), 504–538.

Iwoketok, E. U. (2009). Analysis of lullabic songs in traditional African communities: Some Nigerian examples. *African Research Review: An International Multi-Disciplinary Journal, 3*(3), 147–157.

Janaki, V. (2021). Multidisciplinary research in the social sciences: Breaking new grounds. *Journal of Mind and Society, 10*(3–4), 134–138.

Kipkorir, L. I. (1987). Innovation in early childhood education and care: The Kenyan experience. In J. Odumbe, E. Agalo, E. Wangui, J. Samali, & W. Eshikhaty (Eds.), *Jadini seminar report* (pp. 52–78). Kenya Institute of Education.

Koski, K., & Savolainen, U. (2016). Genre-text-interpretation: Multidisciplinary perspectives on folklore and beyond. *Finnish Literature Society/SKS*.

Majd, V. K., & Bakhshaliyev, A. (2016). The study of psychological aspects of Iranian mothers' lullabies. *Asian Social Science, 12*(4), 93–100.

Malloch, S., & Trevarthen, C. (2009). *Communicative musicality*. Oxford University Press.

Mbayi, L. A. (2009). *Uhakiki wa fani na maudhui katika tenzi za Howani Mwana Howani na Mwanakukuwa* [Unpublished master's thesis]. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Miyashita, M. (2011). Five Blackfoot lullabies. *Proceedings of the American Philosophical Society, 155*(3), 276–292.

Moon, C. M., & Fifer, W. P. (2000). Evidence of transnatal auditory learning. *Journal of Perinatology, 20*(8, Pt. 2), S36–S43.

Mosweunyane, D. (2013). The African educational evolution: From traditional training to formal education. *Higher Education Studies, 3*(4), 50–59.

Nakin, Z. O. (2021). *The use and value of lullabies and nursery rhymes: A perspective on Isixhosa children's literature* [Unpublished master's thesis]. University of South Africa.

Nettl, B. (2005). *The study of ethnomusicology: Thirty-one issues and concepts*. University of Illinois Press.

Sikora, K., & Żebrowska, B. (2013). Traditional Polish lullabies. In *Estonia and Poland: Creativity and tradition in cultural communication* (Vol. 2, pp. 177–190).

Simiyu, F. W. (2011). *Kitovu cha fasihi simulizi*. Serengeti Publishers.

Standley, J. M. (2002). A meta-analysis of the efficacy of music therapy for premature infants. *Journal of Pediatric Nursing, 17*(2), 107–113.

Sugiyama, M. S. (2001). Narrative theory and function: Why evolution matters. *Philosophy and Literature, 25*(2), 233–250.

Ulutas, M. (2022). An evaluation of the contributions of the words frequently used in Turkish lullabies to language education and development. *International Online Journal of Education and Teaching, 9*(4), 1428–1443.